

**MKATABA WA KUPANGISHA KIWANJA
KILICHOPO KITONGOJI CHA ITUMBI ENEO
LA KATA YA MATUNDASI WILAYA YA
CHUNYA MKOA WA MBEYA**

KATI YA

BW. TOMGEMS COMPANY LIMITED

NA

**BW:
NINGSHENG MINERAL PROCESSING CO., LTD**



**MKATABA WA KUPANGISHA KIWANJA KILICHOPO
KITONGOJI CHA ITUMBI ENEO LA KATA YA MATUNDASI
WILAYA YA CHUNYA MKOA WA MBEYA**

MKATABA HUU UMEFIKIWA Leo tarehe 12 Mwezi 07 2024

KATI YA

BW: TOMGEMS COMPANY LIMITED kampuni ambayo imesajiliwa chini ya sheria ya makampuni sura ya 212 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 (the Companies Act, Cap. 212 RE 2002) ya sanduku la posta nambari 11190 Arusha Region, Tanzania (ambac katika Mkataba huu anatajwa kama "Mwenye Kiwanja" kwa upande mmoja

NA

NINGSHENG MINERAL PROCESSING CO.,LTD, CHUNYA Nambari za simu 0683467545 Mkazi wa Itumbi (ambaye katika mkataba huu anatajwa kama "Mpangaji") kwa upande mwingine.

KWAMBA: Mwenye Kiwanja ni mmiliki halali wa Kiwanja kilichopo Kijiji cha Matundasi Kitongoji cha Itumbi Halmashauri ya Mji Mdogo wa Makongolosi Wilaya ya Chunya Mkoa wa Mbeya na Kwahiyari yake Mwenyewe ameridhia kumpangisha "Mpangaji" kiwanja husika na yeye "Mpangaji" ameridhia kupanga kiwanja husika kama kilivyo.

KWAMBA: Kiwanja kinachopangishwa kipo katika majira ya nukta kama ifuatavyo:-

08' 22' 24" 5	33' 18' 48" E
08' 22' 24" 5	33' 18' 38" E
08' 22' 18" 5	33' 18' 48" E
08' 22' 18" 5	33' 18' 38" E

TOMGEMS COMPANY LIMITED
12 JUL 2024
P.O. BOX 11190
ARUSHA

NA KWA KUWA Mwenye nyumba amehiari kumpangisha Mpangaji naye Mpangaji amehiari kupanga Kiwanja hiyo kama kinavyo jionyesha katika majira ya nuka hapo juu.

Witness:
12/07/2024

Richard Ally Baruti
Advocate, Notary Public
& Commissioner for Oaths

[Handwritten signature]

HIVYO BASI MKATABA HUU unathibitisha kuwa mpangishaji na Mpangaji wamekubaliana kama ifuatavyo:

1. Kwamba malipo ya kodi ni **T.Shs. 2,500,000/=** (Shilingi Milioni Mbili na Laiki Tano Tasilimu) kwa mwezi ambapo Mpangaji atatakiwa kulipa fedha za miezi Miwili (02) ambazo ni. **T.Shs. 5,000,000/=** (Shilingi Milioni Tano Tasilimu).
2. Kwamba, Mwenye Kiwanja anakiri kupokea kiasi cha Shilingi Milioni Kumi na Tano Tasilimu (Tshs. 15,000,000/=) ambayo ni kodi ya kiwanja ya miezi Sita kuanzia tarehe 12/07/2024 hadi tarehe 12/01/2025.
3. Mpangaji anaahidi kwa dhati kuwa:
 - (a) Atalipa kodi ya pango kwa namna ilivyoelezwa hapo juu.
 - (b) Atakuwa huru na mwenye haki zote za upangaji mradi kwamba atatimiza masharti yafuatayo:
 - Analipa kodi kama alivyokubaliana na mwenye Kiwanja.
 - Hatachafua wala kuharibu mazingira ya Kiwanja alichopangishwa
4. Nae Mwenye Kiwanja anaahidi kwa dhati kuwa:

atamwacha Mpangaji akiitumia Kiwanja alichopanga kwa raha mustarehe bila bughudha yoyote kutoka kwake au kwa mawakala wake au mtu yeyote mwingine mradi tu Mpangaji anatekeleza masharti yaliyomo katika mkataba huu.

 - (a) Mwenye Kiwanja atawajibika kufanya mambo yafuatayo:-
 - Mwenye Kiwanja atawajibika kulipia kodi ya Kiwanja inavyotakiwa kila mwaka kisheria.
5. Mwenye Kiwanja na Mpangaji wanakubaliana pia kama ifuatavyo:
 - (a) Kila baada ya muda ya Malipo ya kodi ya upangaji wa Miezi Miwili (02) "**Mwenye Kiwanja**" atasaini makubaliano kukiri kupokea malipo ya kodi husika.

- (b) Kwamba, "Mwenye Kiwanja" akivunja mkataba wakati wowote ambapo mkataba huu uko hai yaani haujafikia ukomo basi atalazimika kumlipa "**Mpangaji**" gharama za uwekezaji katika kiwanja hicho.

Kwamba mkataba huu utakuwa ni wa Kipindi cha Miaka Kumi na Tano (15) na utanza kutumika tarehe 12/07/2024 hadi tarehe 12/07/2039.



Wassiyi
12/07/2024



- (d) Kwamba, iwapo kama "Mpangaji" atachelewesha kulipa kodi ya Kiwanja kwa kwa kipindi cha zaidi ya siku saba (07) kuanzia tarehe yake ya kufanya malipo ya kodi basi "Mwenye Kiwanja" atamtoza riba ya asilimia 25% ya kodi ya kiwanja.
- (e) Kwamba Mwenye Kiwanja hatamtambua mtu mwingine kuachiwa upangaji na Mpangaji kinyume cha mkataba huu.

KWA KUTHIBITISHA YALE YOTE YALIYOMO NDANI YA MKATABA HUU,

Mwenye Kiwanja na Mpangaji wameweka saina zao hapa chini katika tarehe iliyotajwa hapa chini.

Umeshuhudiwa na Umetiwa saina hapa Chunya na **BW. TOMGEMS COMPANY LIMITED** ambae ametambulishwa kwangu na..... ninayemfahamu leo tarehe ...12../...07..../ 20..24



MBELE YANGU:

.....
WAKILI

Umeshuhudiwa na Umetiwa saina hapa Chunya na **BW. NINGSHENG MINERAL PROCESSING CO. LTD**..... ninayemfahamu leo tarehe ...12../...07..../ 20..24

MPANGAJI

MBELE YANGU:

.....
WAKILI

Umeandaliwa Na:
 Mwenye nyumba.
MBEYA.